

Swali: Kughafilika maana yake nini?

Jibu: Turejee...

Wagalatia 6:1 “Ndugu zangu, mtu akighafilika katika kosa lo lote, ninyi mlio wa Roho mrejezeni upya mtu kama huyo kwa roho ya upole, ukijangalia nafsi yako usije ukajaribiwa wewe mwenyewe.

2 Mchukuliane mizigo na kuitimiza hivyo sheria ya Kristo”

Kughafilika maana yake ni **“Kuchukuliwa na jambo fulani baya”..** Mtu aliyeghafilika anakuwa amezama katika Uovu na anakuwa haoni tena kama ni kosa kufanya uovu ule (*kiasi kwamba ufahamu wake unakuwa kama umefungwa*)..

Kwamfano mtu aliyezama katika anasa ambao hapo kwanza alikuwa anaukataa, mtu huyo anakuwa **“Ameghafilika katika anasa za dunia”** n.k

Biblia inatufundisha kuwa watu kama hawa ni kuwarejesha kwa roho ya upole, Maana yake kwa kuwafundisha taratibu na kuwaombea mpaka watakaporudi katika mstari, na hiyo ndiyo tafsiri ya kuchukua mzigo wa mwingine, (*yaani ni kumrejesha katika kweli, mtu aliyekengeuka, na si kumwombea baada ya kufa!*)

Mtu aliyekufa hakuna mtu anayeweza kuuchukua mzigo wake wa dhambi, bali atasimama nao mbele ya kile kitie cha hukumu..

Wagalatia 6:5 “Maana kila mtu atalichukua furushi lake mwenyewe”

Na sio tu mtu, bali hata Bwana mwenyewe hatamchukulia mtu mzigo wa dhambi, baada ya kifo....

Yohana 8:21 "Basi akawaambia tena, Mimi naondoka, nanyi mtanitafuta; NANYI MTAKUFA KATIKA DHAMBI YENU; mimi niendako ninyi hamwezi kuja.....

24 Kwa hiyo naliwaambieni ya kwamba MTAKUFA KATIKA DHAMBI ZENU; kwa sababu msiposadiki ya kuwa mimi ndiye, MTAKUFA KATIKA DHAMBI ZENU".

Je umeokoka?.. una uhakika Bwana YESU akirudi leo utakwenda naye?.

Maran atha..

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kughafilika ni nini? (Wagalatia 6:1)

Kwa mawasiliano: +255693036618 au +255789001312

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

Uchambuzi na Mwandishi wa kitabu cha Wagalatia

WALIPO WAWILI AU WATATUS KWA JINA LANGU

Je, kama hauna ubatizo sahihi hauwezi kuwa na Roho Mtakatifu?

Ni uchafu gani unaozungumziwa katika Wagalatia 5:19?

je! Paulo aliwalaani Wagalatia na Wakorintho?

Rudi Nyumbani

Share on:

WhatsApp